SEPTEMBA 2024



# compass

The Salvation Army's Global Strategic Framework

People • Mission • Legacy

'Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika, ila natenda neno moja tu, nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele, nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.'

(WAFILIPI 3:13-14).



# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Kutoka kwa Jenerali | 03 |
| Historia na Siku za Mwanzo | 04 |
| Utume wa Makao Makuu ya Kimataifa | 05 |
| Compass ilianzishwa namna gani ? | 05 |
| Safari Inaendelea | 06 |
| Maono ya Compass | 08 |
| Maeneo Matatu ya Kuzingatia | 09 |
| #1 Kuwawezesha Watu | 10 |
| #2 Kuimarisha Mguso wa Utume | 12 |
| #3 Kuanzisha Urithi Unaodumu | 14 |
| Nini Kinahitajika ili Kupata Mafanikio? | 18 |
| Uwajibikaji na Mguso | 19 |
| Mwisho | 20 |
| Muhtasari wa Compass | 21 |

# Kutoka kwa Jenerali



'Maono yangu ni kwa ajili ya kila sehemu ya Jeshi la Wokovu isiombe msamaha kuhusu kujiamini kwake kuhusu injili ya Yesu Kristo ya kubadilisha maisha na kupatanisha wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, na kumbatio la upendo la Baba yao wa mbinguni.'

Salaam! Namshukuru Mungu kwa sababu ya mchango wa thamani mnaoutoa kwa maisha ya Jeshi la Wokovu. Natumaini nia na mioyo yenu itatiwa moyo, itapata changamoto na kuhamasishwa kutenda kazi mnaposoma Compass: Mfumo wa kazi wa Mkakati wa Jeshi la Wokovu Duniani.

Tumebahatika kuwa sehemu ya Jeshi la Wokovu la Mungu. Sisi ni kundi kubwa la mchanganyiko wa watu lililojitoa kumpenda Mungu na kuwapenda watu. Tunatoa huduma katika nchi 130 duniani. Tunakabiliana na changamoto mbalimbali na mara nyingi tunapita katika maji yenye matatizo. Kwa hiyo, viongozi wenu wa kimataifa na wale wa kiteritori wamekuwa katika safari miaka miwili iliyopita ili kutambua changamoto kubwa zinazokabiliwa na Jeshi la Wokovu duniani.

Mfumo wa kazi wa Mkakati huu Duniani unatumia taswira ya dira kwa sababu tunatoa kwa kila sehemu ya Jeshi letu mwelekeo ulio wazi kwa ajili ya utendaji kulingana na vipaumbele 12. Ni wajibu wangu kama Jenerali wenu kusikiliza ile hekima na uzoefu wa viongozi wa teritori na wa kimataifa, kuwasikiliza watu wengine wengi ambao maoni yao nayapokea na kisha, kwa umuhimu kabisa, kuleta sauti zote hizi mbele za kiti cha enzi cha Mungu na kutambua mwelekeo ambao Mungu anataka Jeshi lake liuendee.

Sasa tuko tayari kuwashirikisha ninyi vipaumbele hivi 12 (tazama muhtasari ulio mwisho wa taarifa hii). Jeshi la Wokovu duniani lina baadhi ya changamoto hizi za kawaida – kama ruzuku ya afisa, ambayo ni hitaji kubwa sehemu nyingine duniani kuliko nyingine.

Maneno matatu yanabeba vipaumbele vyote 12:

- Watu
- Utume
- Urithi

Ingawa tunaanza katika maeneo mbalimbali tofauti, sote tunatakiwa kuhakikisha tunawajali watu wetu, tunaendeleza utume wetu na tunaacha urithi unaomheshimu Mungu. Tunahitaji kujenga kasi kote ndani ya Jeshi – katika ngazi zote – kuhakikisha kila kikao, kituo, mpango na makao makuu yanazingatia kuhakikisha watu wetu wamewezeshwa kuendeleza utume wa Mungu na tunaacha urithi wenye misingi imara kwa ajili ya siku zijazo.

Compass: Mfumo wa kazi wa Mkakati Duniani utatusaidia sisi kuyafanya haya. Hata hivyo, Compass hailengi kumbana kila mmoja awe na umbo moja. Compass inahusu maswali ya kusaidia kuamua mwelekeo wetu badala ya kutoa majibu yaliyoandaliwa.

Hii ni kwa makusudi. Makao Makuu ya Kimataifa inatambua kazi muhimu inayofanywa kuendeleza na kubeba mikakati ya kiteritori.[1] Waraka huu hauchukui nafasi ya mikakati na maono ya teritori ambayo tayari yapo duniani. Hata hivyo, inatoa muundo ambao mikakati ya teritori na utendaji wake unaweza kuendeshwa na kupimwa nao.

Maono yangu ni kwamba kila sehemu ya Jeshi la Wokovu iwe, kwa neema ya Mungu, wazi kuhusu utume wake duniani na wasiombe msamaha kuhusu kujiamini kwao katika injili ya Yesu Kristo ya kubadilisha maisha na kupatanisha wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, na kumbatio la upendo la Baba yao wa mbinguni.

Kutolewa kwa Compass ni hatua nyingine katika safari yetu ya kuhakikisha Jeshi la Wokovu linawezeshwa na linauwezo wa kushiriki katika utume wa Mungu kwa dunia katika karne ya 21 na kupita hapo. Baadhi ya changamoto zitachukua miaka mingi kutatuliwa, lakini kwa nguvu za Mungu tunasonga mbele kwa kujiamini kuelekea kwenye lengo ili tushinde zawadi ambayo Mungu ametuitia. Uwe ni kiongozi wa teritori, kiongozi wa divisheni, kiongozi wa kikao au kituo, uwe na uhakika wa maombi yangu unapotumia Compass katika eneo lako la wajibu.

**Jenerali Lyndon Buckingham**
**Kiongozi wa Kimataifa**

[1] Katika Jeshi la Wokovu, neno 'teritori' linahusu sehemu ya nchi au nchi kadhaa zilizounganishwa pamoja ambapo Jeshi la Wokovu limepangwa chini ya uongozi wa kiongozi mkuu wa teritori.




# Historia

Wakati William na Catherine Booth walipoanzisha kazi mjini London ambayo itakuja kuwa Jeshi la Wokovu, wachache wangeweza kutabiri urithi wao: shirika, sehemu ya Kanisa la Kikristo, sasa linafanya kazi ndani ya nchi zaidi ya 130, likiwa na historia inayozungukia zaidi ya miaka150. Katika muda wote huu, pamekuwepo na kuanzishwa makanisa maelfu yakiwa na mamilioni ya waumini, na watu wasiohesabika wamesaidiwa duniani – lakini chombo hiki kina mianzo ya unyenyekevu.



# Siku za Mwanzo

Alizaliwa mwaka 1829 huko Nottingham, Uingereza, William Booth alipata imani yake ya Kikristo mapema maishani na akawa mhubiri mashuhuri wa Methodisti, akihubiri na kuwasaidia masikini katika eneo lake la nyumbani. Baada ya muda wa kufanya kazi kama mkopeshaji kwa kubadilishana na vitu, alioa na akahama na mkewe Catherine (née Mumford) mashariki ya London. Walianza kufanya kazi na kikundi cha wafanya biashara Wakristo waliokuwa wanahusika na masikini na waliosahaulika katika jamii yao. Juni mwaka 1865, William Booth alihubiria mikusanyiko ya watu nje ya baa ya 'Mwombaji Kipofu – Blind Beggar' pub. Matokeo yalikuwa kuzaliwa kwa chombo kipya kilichoinuliwa na Mungu. Utume wa Kikristo (The Christian Mission) haraka ilizaliwa.

Mwaka 1878, Utume wa Kikristo (The Christian Mission) ikapata jina jipya. William Booth alipinga maneno yaliyokuwemo katika ripoti ya mwaka huo: 'Utume wa Kikristo...ni Jeshi la Kujitolea.' Kwa kubadilisha neno 'kujitolea' na kuweka neno 'wokovu', Jeshi la Wokovu likawa na jina jipya – uwakilishi uliovuviwa kuhusu wajibu wake katika mapambano dhidi ya yasiyohaki katika jamii na kuwaleta watu wamwelewe Mungu. Muda ulipopita, shirika likapata mtindo wa kijeshi (kwa mfano wachungaji wakaitwa 'maafisa',) na hata sare au mavazi yakatengenezwa kudhihirisha kwa watu kujitoa kwake Mungu.

Licha ya tofauti kati ya Jeshi la leo na lile la mwaka 1865, shirika linaendelea kumpenda Mungu na kuwa la kweli kwa watu na mazingira yao. Roho ile ile ya kuweka katika matendo injili ya Yesu, kama ilivyokuwa siku za mwanzoni, inaendelea katika ibada za kila juma, matukio ya nje, makundi na shughuli, kuitikiwa wakati wa majanga na kutoa msaada kimatendo kwa wale wanaohitaji msaada.

# UTUME
## wa Makao Makuu ya Kimataifa

Makao Makuu ya Kimataifa (IHQ), yaliyoko London, Uingereza, yapo ili kumsaidia Jenerali kukamilisha utume ambao Jeshi la Wokovu limepewa na Mungu duniani wa kuhubiri injili ya Yesu Kristo na kukabiliana na mahitaji ya wanadamu katika jina lake bila ya ubaguzi.

Katika kufanya hivyo, inamsaidia Jenerali:

- kutoa uongozi wa kiroho, kukuza maendeleo ya maisha ya kiroho ndani ya Jeshi, na kusisitizia Jeshi kumtegemea Mungu ili kupata utume wake.
- kutoa uongozi mkuu wa kimkakati na kutengeneza sera za kimataifa.
- kuelekeza na kusimamia utendaji wa Jeshi na kulinda maslahi yake – kupitia kwa maagizo na mgawanyo wa mamlaka na majukumu na uwajibikaji.
- kuwezesha na kusaidia teritori, kuhimiza malezi ya viongozi wao, na kuhamasisha maono na mipango yao.
- kuimarisha umataifa wa Jeshi, kuhifadhi umoja wake, kusudi lake na roho yake na kudumisha viwango vyake.
- kukuza maendeleo, kupeleka na kushirikishana watumishi kimataifa.
- kukuza maendeleo na kushirikishana rasilimali fedha duniani, na kusimamia fedha za Jeshi kimataifa.
- kukuza ubora katika maendeleo kimataifa na kushirikishana maarifa, ujuzi na uzoefu.
- kuendeleza uhusiano wa Jeshi na mashirika na makanisa mengine.

# NAMNA GANI
## Compass Iliendelea?

Haya yanawakilisha safari ya miaka miwili inayoonyesha uelewa, na dhamira ya kupokea, nguvu za kipekee za kijamii, mtazamo wa sasa wa dini ya taasisi na wasiwasi unaoongezeka wa ugawaji wa rasilimali toshelevu. Haya yamo ndani ya maono ya Jenerali na katika mashauriano na viongozi wa kimataifa.

Compass: Mfumo wa kazi wa Mkakati wa Jeshi la Wokovu Duniani vile vile unaonyesha kwamba ili Jeshi la Wokovu liwe na mguso wenye ufanisi duniani kupitia kwa Mwili wa Kristo, lazima liendeleze mwelekeo mkubwa kwa watu, kuendeleza masharti ya utume na kuanzisha uaminifu wa huduma ambao utastawi kuwa kizazi kijacho.

Compass inaelezea mbinu ya mpango shirikishi wa kutimiza mamlaka ya Jenerali na viongozi wa kimataifa wa sasa wanaowakilisha kazi duniani.

# SAFARI Inaendelea

Kihistoria, Jeshi la Wokovu limekuwa kanisa ambalo limeendana na mabadiliko ya maswala ya utamaduni ya jamii ya wakati na limejitahidi kuleta nafuu ya hali mbaya ya walio katika mazingira hatarishi wakati huo. Kwa mfano, kwa kuhamasishwa na walivyotendewa isivyo haki wanawake na watoto katika kiwanda cha viberiti, na matumizi ya fosforasi nyeupe yenye sumu inayosababisha hali mbaya ya afya, mwaka 1881 William Booth alifungua kiwanda cha kutengeneza viberiti. Alitangaza 'Mishahara ya Haki kwa Kazi ya Haki' na akatumia tindikali salama ya fosiforasi. Katika miaka kumi, kiwanda kikawa kimebadilisha utendaji wake wa hatari. Yalipotimia malengo ya Booth ya kufanya mazingira ya kazi yawe salama na ya haki, alikifunga kiwanda cha viberiti.

Ilivyopita miaka na duniani kote, Jeshi la Wokovu limefungua vituo mamia kwa ajili ya wasichana na wanawake walionyanyaswa, waliotelekezwa au wanaofanya kazi mitaani. Lakini leo, idadi hiyo imepungua sana kwa sababu ya vituo vinavyoendeshwa na serikali na wingi wa hisani unaolenga wasio na makazi na unyanyasaji wa nyumbani. Duniani kote, huduma zinafunguliwa na vile vile zinafungwa, taasisi huanza kwa kukabiliana na hitaji moja la jamii na kisha hubadilika na kukabiliana na mahitaji mengine inapolazimu. Swala ni kwamba safari ya Jeshi la Wokovu ya mabadiliko na maendeleo imekuwa alama toka kuanzishwa kwake, na inaendelea leo.

Katika miaka ya hivi karibuni, Jeshi la Wokovu kimsingi likiendeshwa na Makao Makuu ya Kimataifa limeendelea na safari yake ya mabadiliko.

### Vipaumbele vya Dunia

Mwaka 2019, Jenerali Brian Peddle alitambulisha 'Vipaumbele vya Dunia', ambavyo vilizingatia maswala 11 ya kuhusika kwa Jeshi la Wokovu. Vipaumbele hivi vilielezea maswala kama miongozo ya upanuzi wa shirika, maboresho ya Microsoft 365, msaada wa UVIKO-19, maendeleo ya utawala na uongozi.

Majira ya chemichemi mwaka 2022, Jenerali Peddle, kwa msaada wa Baraza la Jenerali (TGC),[2] aliitisha uundwe Muungano Unaoongoza (mwenyekiti wake Katibu Mkuu wa Kimataifa). Kusudi la Muungano Unaoongoza lilikuwa na mambo mawili: kuhakiki maendeleo yaliyopatikana katika vipaumbele vya mkakati 11 vilivyopendekezwa na Jenerali Peddle, na kutambua mikakati mipya ya vipaumbele kwa ajili ya siku zijazo. Majukumu haya yaliidhinishwa na Baraza la Jenerali na Kampuni ya Udhamini ya Kimataifa ya Jeshi la Wokovu ((SAITCo).

Katika mkutano wa  Baraza za Ushauri la Jenerali[3] (GCC55) (23-25 Mei 2022), Jenerali Peddle aliendeleza uchunguzi wa mabadiliko ya mkakati. Katika hotuba yake ya msingi, Jenerali anaelekeza maswali yafuatayo:

- Je, maafisa na askari wanafahamu kwa uwazi na wameunganishwa kutambua kwanini tuko hapa?
- Vikwazo vya maendeleo ya utume ni vipi na tunaweza kuvisimamia namna gani?
- Ni matendo gani yanayohitajika ili kubadilisha mitindo na kuzaa matunda?
- Je, imani yetu ni wazi kuhusu mamlaka ya maandiko?
- Katika dhana ya utamaduni/Kikristo, je, tunaelekea katika mwelekeo sahihi?
- Je, sisi, kwa kweli, tunazingatia ipasavyo uaskari kama kipengele cha msingi cha nguvu yetu na uwezo wetu wa siku zijazo?

Kisha alitengeneza maelezo haya, 'Napendekeza kwenu kwamba japo nasimamia mazingira mengi, tunarudi mara kwa mara kwenye mkakati wetu kuzungukia vipaumbele vya msingi. Kushindwa kokote kufanya hivyo kunapendekeza kuliweka Jeshi katika hatari nami naomba tusifanye hivyo.

Kuliweka Jeshi la Wokovu katika hatari kwa kushindwa kukabiliana na maswala muhimu ya leo ni hatari ambayo haiwezi kupuuzwa. Kwa hiyo, kazi ya ziada ilifanywa ili kuamua hali ya vipaumbele 11 vya Dunia vya nyuma na, chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Kimataifa (Kamishena Lyndon Buckingham), vipaumbele vilivyorekebishwa vilitengenezwa kwenye Mkutano wa Viongozi wa Kimataifa (ICL) mwaka 2022. Vipaumbele vipya kumi na tano vilitengenezwa vilivyowakilisha fikra ya pamoja ya viongozi wote wa kimataifa wa siku ile.

[2] Baraza la Ushauri la Jenerali (TGC), lililoanzishwa mwaka 1991, hutoa ushauri kwake Jenerali katika kuongoza Jeshi la Wokovu. Lina makamishena walioutumishini walio Makao Makuu ya Kimataifa, London na Katibu Mkuu, na hukutana kila mwezi huku Jenerali akiwa mwenyekiti.

[3] Baraza la Ushauri la Jenerali, lililoanzishwa mwaka 1991, lilimshauri Jenerali katika maswala mtambuka yanayohusu mkakati wa utume na sera ya Jeshi. Watu waliochaguliwa hukutana kwa ajili ya mikutano, sio zaidi ya mara tatu kwa mwaka, chini ya uenyekiti wa Jenerali.



## Compass: Global Strategic Framework

Kufuatia kuchaguliwa kwa Jenerali mpya, mikutano ya ziada ya viongozi wakuu (GCC56 4-6 Septemba 2023 na GCC57 18-20 Machi 2024) ilifanyika. Jenerali Buckingham alielekeza ushiriki uendeleze kazi ya pamoja ya kuboresha jinsi Jeshi litakavyoonekana miaka ijayo. Waraka huu unawakilisha matokeo ya Mabaraza ya Ushauri ya Jenerali katika Compass yaliyoidhinishwa: Mfumo wa kazi wa Mkakati wa Dunia.

Tunapoangalia maswala ya Jeshi la Wokovu hivi leo, na vipaumbele vipya vilivyotambulika na viongozi duniani, ni dhahiri kwamba mabadiliko ya kupokelewa – mabadiliko ambayo yatahitaji uvumilivu, kuchukua tahadhari na ushirikiano kwa muda – yatahitajika. Ushindi utahitaji mabadiliko katika akili na mioyo ya watu. Ufumbuzi hautaonekana mara moja. Bali utajitokeza tunapoomba, kwa uvumilivu na tunapofuatilia mapema utendaji mpya, mifano mipya ya huduma na kudumisha uelewa wa mara kwa mara wa uongozi wa Roho Mtakatifu.

## Nani anayekusudiwa na Haya?

Waraka huu umekusudiwa kufahamisha umma kuhusu mwelekeo wa kimkakati ambao Jeshi la Wokovu litauzingatia kwa miaka mitano ijayo. Unawakilisha hamu ya Jenerali ya kutoa mwelekeo wa dunia. Unaleta pamoja kazi ya miaka mingi ya mazungumzo, maombi na maandalizi. Habari inayofuata inaelezea mfumo ambao kwa upana unatoa muhtasari wa mwelekeo wa utume wa Jeshi la Wokovu na huduma yake kwa umma. Hata hivyo, haibainishi jinsi teritori binafsi itapanga shughuli zake ziendane na mpango huu.

Hakuna jitihada za kupunguza kazi muhimu ambayo kwa sasa inafanywa kuendeleza na kuendesha mikakati ya kitaifa. Compas haiji kufunika mikakati na maono ambayo yapo duniani tayari. Hata hivyo, inatoa muundo ambamo kazi duniani zinaweza zipangwa ziandane nayo kimkakati. Kama kiongozi mmoja wa teritoti alivyosema: 'Sisi sote tumo katika magari katika barabara ile ile. Sasa tunafahamu mwelekeo na tunakotaka tufike.'

Kwa kuongezea, inaeleweka kwamba nchi zingine zitazingatia maeneo fulani maalum ya mfumo kwa sehemu kubwa kuliko wengine. Hii inaeleweka. Lakini uelewa wa maeneo yote ya mfumo huu, pamoja na ushirikiano ili kukamilisha malengo na uwajibikaji ili kuonyesha ushindi, itakuwa lazima.

# Tamko la Utume la Kimataifa

Jeshi la Wokovu, chombo cha kimataifa, ni sehemu ya uinjilisti ya Kanisa la Kikristo duniani. Msingi wa **ujumbe** wake ni Biblia. Huduma yake inahamasishwa na upendo wa Mungu. **Utume** wake ni kuhubiri injili ya Yesu Kristo na kukabiliana na mahitaji ya wanadamu kwa jina lake bila ubaguzi.



## Tamko la Kusudio la Compass

**Kuwashirikisha wengine upendo na kazi ya Mungu inayobadilisha kwa maneno na matendo.**

# MAONO ya Compass

**Tuna maono ya Jeshi la Wokovu duniani lililofanywa upya la watu waliowezeshwa, waliopewa vifaa ili wawashirikishe wengine upendo wa Kristo na uwezo wa Mungu unaobadilisha ndani ya jamii kote duniani.**

# Maeneo
## MATATU ya Kuzingatia

Baraza la Jenerali (TGC), Kampuni ya Udhamini ya Jeshi la Wokovu Kimataifa (SAITCo) na Baraza la Ushauri la Jenerali (GCC) walichukua maeneo matatu ya kuzingatia (tazama hapo chini) yanayotoa mfumo kwa maafisa na askari wote wa Jeshi la Wokovu wanapotafuta kuwezesha mguso wa chombo hiki duniani.

Kwa kuongezea maendeleo ya mfumo unaoendana na historia, utume na maono ya siku zijazo za Jeshi la Wokovu, tunakiri kwamba mifumo ya mikakati na vipaumbele vya nyumbani na vipo mezani kote katika duniani ya Jeshi la Wokovu. Mkakati huu hauna lengo la kufutilia mbali kazi zilizofanywa mapema ndani ya teritori duniani, bali utatoa mwelekeo wa mkakati ambao utaelekeza teritori pamoja katika utume wa ushirika na kuelekeza kule ambako rasilimali na vifaa vitaelekezwa.

1. Kama Jeshi duniani tumedhamiria **Kuwawezesha Watu**
2. Kama Jeshi duniani tumedhamiria **Kuimarisha Mguzo wa Utume**
3. Kama Jeshi duniani tumedhamiria **Kuanzisha urithi Udumuo**

**Sehemu zifuatazo zitatoa mitaro ya Maeneo ya Kuzingatia, sio kiwango na kina kamili cha kila kipengele.**



# 1 Kuwawezesha Watu

Kwa kutambua umuhimu mkubwa wa kuwapa viongozi vifaa na mafunzo ya huduma, kujenga Mwili wa Kristo kupitia kwa vikao na vituo vyetu, na kuwaweka katika msingi wale wote wanaohusika na huduma yetu, wapate uelewa wa msingi wa hamasisho letu na utekelezaji wa utume wetu, tutachukua hatua, tutaelekeza rasilimali na kutoa mafunzo na kutoa nafasi za mafunzo ili **Kuwawezesha Watu** sawa na kazi yetu.

## KWA NINI NI MUHIMU

- kwasababu makusanyiko ya waumini lazima yatafute maisha matakatifu na matendo ya haki kibiblia.
- mafunzo bora na kuwawezesha viongozi vitasaidia huduma na wajibu mkubwa.
- kusisitizia kanuni za utakatifu za Wesley kunathibitisha thamani yetu ya theolojia na kusaidia kujitoa kwetu kuishi maisha matakatifu.
- kuzamisha ndani uinjilisti na nidhamu ya uinjilisti vitaendeleza kujitoa kwetu kuwa watu wa 'Wokovu'.
- kuwahimiza watu wetu wauishi utume wetu kutaimarisha jamii na makusanyiko ya waumini.
- kuhakikisha waajiriwa na wanaojitolea wanaelewa ushawishi wa Kikristo na matendo ya utume wetu.

## MATOKEO YANAYOTARAJIWA

- vyuo vya mafunzo kupewa rasilimali zinazoendana na za lugha sahihi ya kuwafundisha maafisa kwa ufanisi zaidi.
- mtazamo mkubwa zaidi wa teritori kuhusu utamaduni wa Jeshi la Wokovu kuhusu utakatifu na matendo.
- uchapishaji wa mara kwa mara na uratibu wa nyenzo za rasilimali, kama vile nidhamu ya kiroho, utofauti wa Jeshi la Wokovu, vitambulisho vya Jeshi la Wokovu na nyenzo za malezi ya kiroho kwa vijana.
- ukuaji mkubwa wa waumini na utoaji wa mipango jumuishi ya utume.
- mikusanyiko zaidi ya waumini inayokaribisha na inayojihusisha na maswala ya jamii.
- maongezeko ya idadi ya wafanya kazi na wanaojitolea wanaoelewa na kukumbatia maono ya Jeshi la Wokovu, utume na maadili yake.

## KUJIHUSISHA KWA MAKAO MAKUU YA KIMATAIFA (IHQ)

Mkakati huu utaundwa na kuratibiwa na Makao Makuu ya Kimataifa kwa sababu wanazingatia utendaji duniani, sera na msaada wa watendakazi waliopewa majukumu hivi karibuni ulioidhinishwa na Jenerali:

- uelewa na mazungumzo ya ujinsia wa binadamu
- maendeleo na mgawanyo wa nyenzo za rasilimali
- baraza la Theolojia la Kimataifa
- mafunzo ya Maafisa Kimataifa na Baraza la Maendeleo ya Kiongozi
- ukuaji endelevu wa Maisha ya Kiroho Kimataifa na sehemu za Maendeleo ya Uongozi.

## JINSI TUTAKAVYOFANYA

Mifereji minne itakabiliana na kusudi la Eneo hili la Kuzingatia na kufikiria maswala ya msingi yaliyo muhimu kwa mtiririko wa kazi, vile vile kufanya mapendekezo kwa Jenerali ili hatua zichukuliwe. Hata hivyo, habari zifuatazo zitazingatia mtiririko wa kazi ambao utakuwa na mguso kwa umma.

### 1) Maisha ya Kiroho

- kuanzishwa kwa Makatibu wa Maendeleo ya Maisha ya Kiroho katika kila teritori duniani, ambao kimatendo wanatoa kipaumbele cha afya njema ya kiroho ya Jeshi la Wokovu na waumini wake.
- teritori zinashiriki katika kushirikishana rasilimali na kwa makusudi wanashirikishana mawazo
- matumizi ya mara kwa mara ya njia za mawasiliano zilizoandaliwa na Makatibu wa Maendeleo ya Maisha ya Kiroho.
- waumini wa Jeshi la Wokovu kushiriki kikamilifu katika mipango muhimu ya kimataifa inayotekelezwa na Jeshi la Wokovu.
- kuongeza uelewa wa utamaduni wa utakatifu wa Jeshi la Wokovu kupitia kwa semina na taasisi za Brengle, na maisha ya kuuishi utakatifu.
- kuongeza ushiriki wa washiriki katika maombi kupitia kwa mipango ya Mikutano ya Maombi Duniani.
- utekelezaji wa mipango na miradi inayoendana na utume wa Jeshi la Wokovu katika teritori zote.
- ushahidi wa ukuaji wa kiroho na mabadiliko yanayoweza kupimwa, yaliyodhihirishwa kupitia kwa shuhuda binafsi, mabadiliko ya tabia na mguso wa huduma.
- maafisa, askari na viongozi wanayaishi maadili na wamejitoa kuendeleza utume na maadili ya Jeshi la Wokovu.

**Lengo: Kuimarisha kina cha kiroho na kujitoa kwa utakatifu kati ya Waumini wa jeshi la Wokovu na kudumu katika kweli ya utume wetu na utambulisho wetu kama Jeshi la Wokovu.**

**Viashiria vya Mafanikio:**

- wale wanaoshiriki katika huduma za Jeshi la Wokovu watatafuta kuishi katika njia ya kufanana na Kristo zaidi.
- Waumini wa Jeshi la Wokovu, wafanyakazi, wanaojitolea na marafiki wa Jeshi la Wokovu watazaa matunda makubwa kwa Ufalme wa Mungu.
- wale wote wanaohusika na huduma za Jeshi la Wokovu watagundua na kushirikisha karama zao za rohoni katika kuwatumikia wengine.

### 2) Maendeleo ya Uongozi

- maendeleo ya mfumo wa kuendelea kujifunza kwa teritori ambazo bado hazijaanzisha hili.
- maendelezo ya kazi kuhusu hazina (na Chuo Kikuu cha Booth) kwa ajili ya misaada ya kuwafundisha wakuu wa vyuo (mwongozo wa kuwafundisha wakuu wa vyuo tayari umeandaliwa na Mafunzo ya Kimataifa kwa Maafisa na Baraza la Maendeleo ya Kiongozi [IOTALDC]) na wafanyakazi wa mafunzo - pamoja na mchango wa vyuo vikubwa katika nyenzo za mafundisho na ushauri wa mtaala.
- maendeleo ya hazina ya jukwaa la elimu ya kujifunza.
- kuanzishwa kwa kikundi cha Maendeleo ya timu za Kiongozi kwa ajili ya kushirikishana rasilimali na kutiana moyo kwa kuheshimiana.
- maendeleo ya Kozi ya Mafunzo ya Uendeshaji kwa Kiongozi kwa ajili ya siku zijazo/wakuu wa idara, ikiwa pamoja na vipengele vya mafunzo vya mtu kwa mtu na vya mtandaoni.

**Lengo: Kuendeleza maafisa ambao ni viongozi watumishi, ambao wamekomaa kiroho, wanajiamini na wamewezeshwa kwa ajili ya maagizo yao ya sasa na yale yajayo.**

**Viashiria vya Mafanikio:**

- viongozi ambao watastawi katika wajibu wao.
- maafisa ambao watahudumu kwa ufanisi katika maagizo ya aina mbalimbali.
- kila kiongozi atazingatia utume.

# 2 Kuimarisha Mguso wa Utume

Mwito kwa kila Mkristo ahusike kimatendo katika utume wa Mungu (*missio Dei*). Kwa mwisho huo Jeshi la Wokovu linachukua wajibu uliodhahiri katika Kanisa leo. Kwa wale wanaoshiriki katika huduma zetu na wanaokisaidia hiki chombo chetu, panahitajika juhudi kubwa za **Kuimarisha Mguso wa Utume**.

## KWANINI NI MUHIMU

- uamuzi wa kuanzisha mifano mipya ya huduma na inayoendana na wakati utatoa ubunifu na ukuaji mpya wa utume.
- maelezo yanayoeleweka wazi ya kuwa mwamini na agano yatasababisha pawepo kujitoa kiroho.
- kuthibitisha, kukumbatia na kuwa wa ndani ni dhana za sasa ambazo zitaleta uwazi kwenye uongozi wa mkusanyiko wa watu wa Jeshi la Wokovu.
- uelewa mkubwa wa vinavyoleta utofauti wa utume shirikishi wa Jeshi la Wokovu utasaidia kuhamasisha mikusanyiko ili wakabiliane na mahitaji ya jamii.

## MATOKEO YANAYOTARAJIWA

- uundwaji wa aina mpya za kuabudu kwa mikusanyiko ndani ya teritori kote duniani.
- kuendeleza uwazi kuhusu marafiki (adherence) na waumini wa kikao.
- kuanzisha uelewa wa kisasa wa agano ili kusaidia kuelezea uafisa na uaskari.
- maendeleo ya 'yasiyoweza kujadiliwa' kuhusu sifa za utambulisho.
- teritori kuwa na uelewa wa wazi wa mahusiano yao na Makao Makuu ya Kimataifa (IHQ).
- wafanyakazi na wanaojitolewa wafahamu wajibu wao katika ukamilifu wa tamko la utume.

## KUHUSIKA KWA MAKAO MAKUU YA KIMATAIFA (IHQ)

- uelewa wa kitheolojia wa mahusiano ya kiagano.
- mazungumzo kuhusu mahusiano kati ya Makao Makuu ya Kimataifa (IHQ) na Makao Makuu ya Teritori (THQ).
- maendeleo ya vikundi vya utendaji kazi vya marafiki (adherence) na waumini.
- mkutano kuhusu ubunifu unaoendeshwa na utume.

## JINSI TUTAKAVYOFANYA

Mitiririko minne ya kazi itakabiliana na makusudi ya Eneo hili ya Kuzingatia na kufikiria kuhusu maswala ya msingi yanayohusu mtiririko wa kazi, pamoja na kufanya mapendekezo maalum kwake Jeneral ili hatua zichukuliwe. Hata hivyo, habari ifuatayo itazingatia tu ile mitiririko ya kazi ambayo itagusa umma.

### 1) Uanachama

Tutachunguza maswali kama: 'Tunaelewaje uanachama na kuwa mtu wa Jeshi la Wokovu hivi leo?' na 'Ni nini kinachowazuia watu kuwa wanachama?'

**Lengo: Kuanzisha uwazi na usahihi katika kuelezea jinsi watu wanavyokuwa sehemu ya ushirika wa Jeshi la Wokovu.**

**Viashiria vya Mafanikio:**

- uwazi kuhusu kuwa mwanachama (muumini) maana yake nini.
- kama neno 'rafiki' (adherent) linafaa leo.
- nani anaweza kuwa mwanachama na kushika nafasi ya uongozi.

### 2) Utume Shirikishi

Utume wetu ni kipengele muhimu cha utambulisho wetu. Kushirikisha huduma yetu ya wokovu binafsi na wa jamii, kuzingatia uinjilisti na ukuaji wa kusanyiko la waumini vitasaidia mtiririko huu wa kazi.

**Lengo: Kuanzisha kanuni za ushirika wa kikao ambazo zitashirikisha utume na kuwezesha ukuaji wa kusanyiko la waumini.**

**Viashiria vya Mafanikio:**

- mikusanyiko ya waumini ambayo itazingatia ubora wa tofauti za huduma ya Jeshi.
- majirani kote duniani wataona Ufalme wa Mungu katika vitendo.
- huduma zetu kikaoni zitashawishika kipekee na mahitaji ya jamii zao.



# 3 Kuanzisha Urithi Unaodumu

**Kuanzisha urithi unaodumu** kunakabiliana na umuhimu wa uwakili mwaminifu na wajibu wa kizazi chetu cha Jeshi la Wokovu kwa ajili ya vizazi vijavyo. Urithi ni kile tunachorithi kutoka kwa watangulizi wetu, urithi ni kile tunachokiachia kizazi kinachotufuata. Jinsi tunavyoendeleza kumtegemea Mungu, jinsi fedha zinavyosimamiwa, jinsi tunavyozidisha umiliki wa pamoja, na jinsi wajibu unavyowekwa dhamana kwa vikao, vituo na jamii - sababu zote hizi zitasababisha urithi wetu na uwezo wa Jeshi la Wokovu wa kutumikia utume wa Mungu siku zijazo.

## KWANINI NI MUHIMU

- Mungu anatutarajia sisi tuwe mawakili wazuri.
- uwakili wa teritori moja kwa moja unahusiana na mgawanyo wa rasilimali chache.
- mikakati ya kukabiliana na mahitaji ya binadamu walio katika mazingira hatarishi zaidi, badala ya mahitaji ya jumla ya binadamu, itasaidia kuelezea kuzingatia mpango.
- kufuatilia kutegemea ufadhili wa kimataifa kutasaidia washirika kusaidia teritori zijitafutie rasilimali.
- kushirikishana watenda kazi kikamilifu kutahakikisha kuna maendeleo ya viongozi na kuna umataifa.
- kujitoa kwa ustawi wa kiroho na vitu wa kila afisa kutaonyesha heshima ya shirika na thamani ya maafisa.

## MATOKEO YANAYOTARAJIWA

- kuzingatia mkakati wa teritori wa sasa na kuanzishwa kwa mipango mipya.
- kushirikishana mafunzo na nafasi za maendeleo kwa viongozi.
- utulivu mkubwa wa teritori kifedha.
- kuzingatia mguso wa Jeshi la Wokovu kwenye mazingira.

## USHIRIKI WA MAKAO MAKUU YA KIMATAIFA (IHQ)

- kuitisha mkutano wa Fedha wa Kimataifa.
- kuendeleza maendeleo ya IFAS, NetSuite na ziara za kusaidia teritori.
- Timu za Kimataifa za Uthabiti.

## JINSI TUTAKAVYOFANYA

Mitiririko minne ya kazi itakabiliana na makusudi ya Eneo hili la Kuzingatia na kufikiria kuhusu maswala ya msingi yanayohusu mtiririko wa kazi, pamoja na kufanya mapendekezo maalum kwake Jenerali ili hatua zichukuliwe. Kazi kubwa katika maswala haya itaratibiwa na Makao Makuu ya Kimataifa.

### 1) Upatikanaji wa Rasilimali

- upatikanaji wa ramani ya ufadhili duniani inayotambua vyanzo mbalimbali vya ufadhili na jinsi inavyotakiwa kutumika kimkakati ili kuendeleza utume kimataifa.
- makubaliano ya kanuni za wazi za ufadhili kwa ajili ya chombo hiki cha kimataifa, pamoja na kusudi na kiwango cha ufadhili.
- mpango ulioanzishwa kwa ajili ya utulivu wa fedha wa siku zijazo wa kila teritori binafsi.

**Lengo: Kuhakiki na kutathmini ugawaji sahihi wa rasilimali za teritori.**

**Viashiria vya Mafaniio**

- msaada wa Makao Makuu ya Kimataifa (IHQ) kwenda kwenye teritoti utahakikiwa na kuthibitishwa.
- teritori zitapata misaada kikamilifu na zitakuwa salama kifedha.
- kila makao makuu ya teritori itajitolea kwa shughuli sahihi za mapato.

### 2) Taasisi

- kumbukumbu ya picha ya taasisi ya msingi katika ulimwengu wote wa Jeshi inayopima mguso wa utume dhidi ya uendelevu (kifedha, rasilimali watu, miundo mbinu, n.k.)
- mkakati wa kuwezesha utulivu wa fedha na mguso wa utume na utoaji wa huduma katika taasisi binafsi, unaofikiria malengo ya utume ya kimataifa na ya kiteritori, mahitaji makubwa ya jamii na uendelevu wa mazingira.
- mkakati wa kukabiliana na uboreshaji au kupanga upya kusudi la taasisi ambazo hazina uendelevu wala si za muhimu kwa utume ili kuhakikisha kuna uboreshaji wa matokeo mengine ya utume.

**Lengo: Kuongeza ubora ndani ya huduma ya taasisi na kupunguza kutegemea ufadhili wa kimataifa.**

**Viashiria vya Mafanikio:**

- uhakiki mpana utadhihirisha mguso wa kifedha wa huduma ya taasisi katika utendaji wa teritori.
- mikakati itaanzishwa kuhakikisha teritori zinaendesha huduma za taasisi kwa ufanisi na kwa matumizi madogo kwenye bajeti ya teritori.
- patakuwa na punguzo muhimu katika hatari za shirika zinazohusishwa na watu walio katika malezi yetu.


SALVATION
ARMY

### 3) Ushirikiano wa Kimataifa

- kukiri umuhimu wa ushirika wa kimataifa na kutambua vipaumbele vya msingi vya ufadhili kuhusu mguso wa utume wa sasa.
- kuanzisha miongozo ya kuimarisha ufanisi na mguso wa utume kutoka kwa ufadhili wa kimataifa wa mradi wa Msaada wa Utume (global Mission Support project funding).
- kutengeneza nafasi za ufanisi za mipango ya uzalishaji wa mapato ili kupunguza kutegemea mapato ya kimataifa.
- kuendeleza mitandao ya kanda ambako teritori zinaweza kushirikiana kutatua matatizo na kujadiliana njia zilizo bora.

**Lengo: Kutengeneza miundo ya mapato inayokabiliana na mapungufu ya bajeti ya kimataifa.**

**Viashiria vya Mafanikio:**

- ufadhili unaosaidia teritori utapangika kimkakati na kugawanywa kikamilifu ili kuhakikisha kuna utulivu wa teritori.
- uzalishaji wa mapato na biashara utaanzishwa ili kuongeza viwango vya mapato ya teritori.
- uwezo utaendelezwa ndani na kimataifa katika watu, taratibu na ushirikiano.

### 4) Makao Makuu yenye Ufanisi

Jeshi la Wokovu linasimamia na kusaidia kazi zake hasa kupitia kwa divisheni, teritori na makao makuu ya kimataifa. Mtiririko huu wa kazi utazingatia utendaji wa Makao Makuu ya Teritori (THQ) duniani.

**Lengo: Kila Makao Makuu ya Teritori (THQ) ina utawala unaofaa kwa kusudi na mfumo wa usimamizi na bajeti inayoendana.**

**Viashiria vya Mafanikio:**

- Makao Makuu ya Teritori yatakuwa na mifumo ya watendakazi inayoendana na bajeti zao na utendaji wao.
- Makao Makuu ya Teritori itakuwa na watendakazi kikamilifu katika nafasi muhimu za ujuzi (m.f. fedha, jamii, chuo cha mafunzo)
- gharama za utawala zitaonyesha kiwango kinachokubalika ukilinganisha na bajeti ya teritori.

# NINI
## Kinahitajika kwa ajili ya Mafanikio?

### 1. MAWASILIANO

Pamoja na mawasiliano yenye ufanisi kwa wadau wote wa mkakati, wakifahamishwa kuhusu wajibu wao na maendeleo yanayopatikana kuelekea kutimiza maono, patakuwa na ushiriki wa wadau, uwazi kuhusu wajibu na taarifa za msaada za wakati zinazoonyesha maendeleo yetu.

### 2. UONGOZI

Viwango vyote vya uongozi lazima kwa makusudi vishiriki katika mfumo wa mkakati ili kuepuka wadau kukata tamaa na kutojali ili kuendeleza makusudi.

### 3. RASILIMALI

Rasilimali za kutosha (muda, watendakazi, fedha) lazima zitengwe ili kukamilisha mfumo wa mkakati ama sivyo tutakuwa tunahatarisha uvumbuzi na kutengeneza mtazamo wa kwamba sisi hatuuchukui mkakati kwa uzito unaostahili.

### 4. KUINGIA

Wote askari, maafisa, wafanyakazi na viongozi lazima wautambue mfumo wa mkakati, na moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja washiriki katika mkakati, kuzuia maendeleo yasipungue na mwishowe kukwama.

### 5. TEKNOLOJIA

Vifaa vya kutosha na msaada wa teknolojia kwa ajili ya mawasiliano (kupitia kwa kiungo cha video, mafaili ya sauti, jukwaa la mitandao ya kijamii) vinahitajika ili kuwafanya maafisa na askari wawe na habari na kutoa uhakika kwamba wanachukuliwa kwa uzito stahiki katika mpango mkakati.

### 6. MAOMBI

Mwisho, lakini bila shaka sio kidogo, mchakato wote huu unahitajika ufunikwe kwa maombi. Lazima kila mara tukumbuke kwamba hili ni Jeshi la Wokovu la Mungu. Sisi ni mawakili kwa majira. Lazima tuhakikishe tunaacha kwa ajili ya kizazi kijacho Jeshi la Wokovu lililojazwa Roho Mtakatifu. Maswala yaliyotambulika katika Compass: Mfumo wa kazi wa Mkakati ni makubwa - zaidi ya uwezo wetu wa kibinadamu. Hata hivyo, kupitia kwa maombi na nidhamu nyingine za kiroho, tunaweza kufuata katika maneno ya Paulo: 'nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele, nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu' (Wafilipi 3:13-14).




# Uwajibikaji na Mguso

Maandishi haya yamepangwa ili yatoe mwelekeo wa kuambatana na mikakati ya teritori yakiwa na matarajio ya wazi kwa ajili ya mwelekeo na vipaumbele vya Jeshi la Wokovu. Yameandaliwa kwa ushirikiano na theluthi moja ya viongozi wa sasa wa teritori na msingi wake ni mashauriano ya Mkutano wa Kimataifa wa Viongozi (ICL) na Baraza la Ushauri la Jenerali (GCC), matokeo yake kila kiongozi wa teritori anaweza kuyapata.

Pakiwepo matarajio ya wazi, kusudi la kawaida na maendeleo ya mkakati wa ushirikiano, kinachohitajika ni uwajibikaji kwa wale walio na majukumu ya kutekeleza mkakati.

Uwajibikaji na mfumo wa mguso utadhihirishwa kwanza katika uhakiki wa teritori na katika ziara za kusaidia teritori. Fomu zinazotumika hivi sasa zitarekebishwa ili zionyeshe mitiririko ya kazi juu ya kurasa hizi. Viongozi wa teritori watatarajiwa kutoa ripoti juu ya viashiria na kutoa vielelezo vya mguso kama inavyostahili.

# Mwisho

Mithali 29:18 inasema:

**‘Pasipo maono, watu huangamia’**

Kwa zaidi ya miaka 155, Jeshi la Wokovu limeweka imani na tumaini lake kwake Mungu adumishe kazi na huduma yake ya kipekee katika Mwili wa Kristo. Tunaendelea kuwa wenye matumaini kwamba licha ya hizi nyakati za changamoto za jamii, uchumi na siasa, umoja wetu, utume shirikishi na kujitoa kiagano vitahakikisha tuna siku zijazo zinazozidi zile zilizopita.

Sehemu muhimu sana ya mkakati ni kujiandaa kuwa tayari kwa changamoto zozote zitakazokuja na kuwa katika nafasi bora ya kukabiliana na changamoto zitakazoletwa na mabadiliko haya. Mpango mkakati huu umeandaliwa kusaidia Jeshi la Wokovu liyapate malengo yake ya mkakati na kuhakikisha pana uendelevu wa shirika. Wakati Compass hii: Mfumo wa kazi wa Mkakati wa Kimataifa unawezesha Jeshi kupanga kwa ajili ya miaka ijayo na kuzitazamia siku zijazo kwa matarajio, uwezo wetu wa kufikia malengo yetu na kuendelea kuigusa dunia kutapimwa kwa sehemu kubwa kwa kujitoa kwetu kwa kanuni hizi na sisi kumtegemea Mungu ‘asiyepimika zaidi’ tunaye mtumikia.

Wengi wetu hatutayaona mabadiliko yatakayotokana na huu mpango mkakati. Yatachukua muda, yatasababisha mifano mipya, taratibu na utendaji, yatakuwa dhihirisho la dhana ya sasa na ile inayochomoza ambamo tunaishi na kutoa huduma. Jeshi la Wokovu litaendelea kuonyesha umuhimu na upekee wake kwa vizazi vya sasa na vijavyo katika kumtumikia Bwana.



compass
The Salvation Army's Global Strategic Framework
People ✦ Mission ✦ Legacy

**Pamoja na Compass (Dira kwa Kiswahili), tumejitoa tuache urithi unaomheshimu Mungu kwa kuyachukua na kuyafanya yetu maeneo matatu ya kuzingatia:**

## KUWAWEZESHA WATU

Watu wapo kwenye moyo wa utume wetu. Tunataka kuhakikisha watu wetu wanaelewa utume wetu na jinsi wanavyoweza kushiriki katika kuufanya utendeke kwa ufanisi zaidi.

## KUIMARISHA MGUSO WA UTUME

Mungu ametupa utume huu - kuhubiri Injili ya Yesu Kristo na kukabiliana na mahitaji kwa jina lake bila ubaguzi. Kwa kufahamu na kuelewa utume wa Mungu, tunaweza kuamini atatuongoza kupita katika siku zijazo zinazoendelea kubadilika.

## KUANZISHA URITHI UNAODUMU

Tutajitahidi kurithisha vizazi vijavyo, Jeshi la Wokovu lenye afya, linalostawi, kwa kuwa mawakili bora wa kila kilichowekwa dhamana katika matunzo yetu.

# 12 VIPAUMBELE

### WATU

1. **Maisha ya Kiroho** – Mfahamu Yesu, uwe kama Yesu, fanya aliyoyafanya Yesu
2. **Maendeleo ya Uongozi** – Kuwaandaa viongozi kwa kuwapa zana wanazohitaji ili wawe na ufanisi
3. **Afya Njema ya Afisa** – Mtazamo makini wa afya ya akili, mwili na roho ya afisa
4. **Fidia ya Afisa** – Kutoa riziki kamili kwa maafisa wote walio uwanjani

### UTUME

5. **Uanachama** – Kuelezea jinsi watu wanavyoweza kuwa sehemu ya ushirika wa Jeshi la Wokovu
6. **Agano** – Kuhakiki agano la askari na la afisa kwa jicho la karne ya 21
7. **IHQ/THQ** – Tathmini mahusiano kati ya Makao Makuu ya Kimataifa na Makao Makuu ya Teritori
8. **Ushirikiano wa Utume** – Kufuatilia mikakati inayoshirikisha vikao na vituo vya kutoa huduma ya jamii

### URITHI

9. **Mgao wa Rasilimali** – Kujitoa kwa ajili ya utulivu wa kifedha wa nyumbani na duniani
10. **Taasisi** – Kuongeza ubora katika utumishi kwenye taasisi.
11. **Ushirikiano wa Kimataifa** – Kuanzisha mifano mipya ya mkakati wa ufadhili ili kuhakikisha utulivu wa kifedha.
12. **Afya ya Utendaji wa Makao Makuu ya Teritori** – Kutengeneza mifumo ya ufanisi itakayokuza utume wetu katika kila teritori